

Muswada wa Haki za Mgonjwa

Muswada wetu wa Haki za Mgonjwa upo kuhakikisha kuwa haki na hadhi ya kila mmoja apataye huduma zetu zinaheshimiwa.

1. Mgonjwa atahudumiwa kwa kuzingatiwa, heshima, na katika utambuzi kamili wa hadhi na ubinafsi wa kila mgonjwa, ikiwa ni pamoja na faragha ya kimatibabu na huduma ya kibinafsi ikiwa ni pamoja na kujulishwa majina, hali ya leseni za kikazi, na vyeo vya wote wamhudumia, kwa mujibu wa RSA 151:3-b.
2. Mgonjwa atapewa habari kikamilifu kuhusu haki za mgonjwa na majukumu na taratibu zote zinazoshughulikia mienendo na majukumu ya mgonjwa. Habari hizi ni lazima zipeanwe kwa usemi na kwa maandishi kabla au wakati wa kulazwa, isipokuwa nyakati za kulazwa kidharura. Mapokezi ya habari hizo ni lazima yakiriwe na mgonjwa kwa maandishi. Mgonjwa akosapo uwezo wa kufanya maamuzi ya kimaarifa, utiaji wa sahihi ni lazima ufanywe na mtu yule aliyepewa wajibu wa kisheria juu ya mgonjwa huyo.
3. Mgonjwa atapewa habari kikamilifu kwa maandishi kwa lugha anayoielewa, kabla au wakati wa kulazwa na wakati atakapokuwa hospitalini kama itakavyohitajika, kuhusu gharama za kimsingi za kila siku na huduma zilizojumlishwa na ambazo hazijajumlishwa kwenye gharama za kimsingi za kila siku. Stakabadhi za huduma ambazo kwa kawaida hazilipiwi na *Medicare* au *Medicaid* pia zitajumlishwa katika ufunuzi huu.
4. Mgonjwa atapewa habari kikamilifu na mtoaji huduma za kiafya kuhusu hali ya ugonjwa wake, mahitaji yake ya huduma za kiafya, na matokeo ya uchunguzi wa kiini cha hali yake, ikiwa ni pamoja na jinsi matokeo hayo yatakavyotolewa na kiasi cha muda unaotarajiwa tangu kupimwa hadi upokeaji wa matokeo, isipokuwa wakati ambapo haifai kufichuliwa kulingana na utaalumu wa kiafya na ikilinganishwa na rekodi za kimatibabu, na atapewa fursa ya kuhudhuria mipango ya kuhudumiwa kwake kwote na matibabu, kukataa matibabu, na kuhusishwa kwenye utafiti wa majaribio wakati pekee atakapokuwa amepeana idhini ya makubaliano yake kimaandishi. Kwa madhumuni ya aya hii "mtoaji huduma za kiafya" yamaanisha mtu yeyote, shirika, kituo, au taasisi iliyopewa leseni aidha katika hali hii au vinginevyo alivyoidhinishwa kisheria kutoa huduma za afya, ikijumlishwa, lakini haija komeshwa kwa, daktari, hospitali au taasisi nyingine ya huduma za kiafya, daktari wa meno, muuguzi, daktari wa macho, podiatristi, mtaalamu wa tiba za kimazoezi, au mwanasaikolojia, na afisa yeyote, mfanyikazi, au ajenti wa mhudumu wa kiafya akitenda kwa niamba na kwa kiwango cha ajira au uajenti uhusishanavyo na au uungavyo mkono huduma za kiafya.

5. Mgonjwa atahamishwa au kupewa ruhusa kurejea nyumbani baada ya mipango ifaayo kwa sababu za kimatibabu pekee, kwa manufaa yake mwenyewe au ya wagonjwa wengine, kama hospitali hiyo itaacha utoaji huduma, au kwa ajili ya kutolipia ukaaji wa mgonjwa, isipokuwa katika jinsi isiyoruhusiwa ikizingatiwa Kichwa XVIII au XIX cha *Social Security Act*. Hakuna mgonjwa atakayelazimishwa kutoka kwa hospitali kwa sababu amepata kuhitimu kuitumia *Medicaid* kama tegemeo la kifedha.
6. Mgonjwa atatiwa moyo na kusaidiwa wakati wote atakapokuwa hospitalini kuzitumia haki za mgonjwa kama mgonjwa na raia. Mgonjwa anaweza kuzisema kero zake na kupendekeza mabadiliko ya sera na huduma kwa wafanyakazi wa hospitali au wawakilishi wa nje bila kuzuiwa, kuingiliwa, kulazimishwa, kubaguliwa, au kulipiziwa kisasi.
7. Mgonjwa ataruhusiwa kusimamia maswala yake binafsi ya kifedha. Kama mgonjwa atairuhusu hospitali kwa maandishi kumsaidia katika usimamizi huu na hospitali ikakubali, usaidizi huo utafanywa kulingana na haki za mgonjwa chini ya kijisehemu hiki na kwa mujibu wa sheria za kitaifa na kanuni.
8. Mgonjwa atakuwa huru kutokana na dhuruma zozote za kihisia, kisaikolojia, kingono na kimwili, na kutokana na unyonyaji, kutelekezwa, adhabu katili ya viboko na kutengwa kwa kutojitolea.
9. Mgonjwa atakuwa huru kutokana na vizuizi vya kemikali na vya mwili isipokuwa wakati wanapopewa idhini hiyo kimaandishi na daktari kwa muda maalumu na mfupi uhitajikao kulinda mgonjwa au wengine kutokana na maumivu. Wakati wa dharura, vizuizi vinaweza kuidhinishwa na mfanyikazi mtaalamu ili kulinda mgonjwa au wengine kutokana na maumivu. Mfanyikazi huyo mtaalamu ni lazima aripoti mara moja kitendo hicho kwa daktari na anakiri hayo katika rekodi za matibabu.
10. Mgonjwa atahakikishiwa hifadhi ya siri ya habari zote za matibabu yaliyomo katika rekodi binafsi ya mgonjwa na ya kikliniki, ikiwa ni pamoja na iliyohifadhiwa kwenye hifadhi atomatiki ya kumbukumbu, na thibitisho pekee la mgonjwa la kimaandishi ndilo litakalohitajika kutoa habari kwa mtu yeyote ambaye hana idhini kisheria kuipokea. Taarifa za matibabu zilizopo katika rekodi ya matibabu kwenye kituo chochote kilichopewa leseni chini ya kifungu hiki itachukuliwa kuwa mali ya mgonjwa. Mgonjwa ana haki ya kupewa nakala ya rekodi kama hizi kama ataiomba. Gharama ya kupewa nakala ya rekodi za mgonjwa haitazidi dola 15 kwa kurasa 30 za mwanzo au dola senti 50 kwa ukurasa, yoyote iliyo zaidi; mradi tu, nakala ya rekodi za kifilamu kama vile rediogramu, mionzi ya X-ray, na sonogramu zitanakiliwa kwa gharama nafuu.

11. Mgonjwa hatatakiwa kufanya huduma zozote kwa kituo. Pafaapo kimatibabu au kwa madhumuni ya kumliwaza na ikikubalika kwake mgonjwa, huduma kama hizo zaweza kujumuishwa katika mpango wa kumhudumia na matibabu.
12. Mgonjwa atakuwa huru kuwasiliana na, kushirikiana na, kukutana kifaragha na mtu yeyote, ikiwa ni pamoja na familia, vikundi vya wenyeji, isipokuwa wakati kufanya hivyo kutaingilia haki za wagonjwa wengine. Mgonjwa anaweza kutuma na kupokea barua za kibinafsi ambazo hazijafunguliwa. Mgonjwa ana haki ya kuweza kutumia mara kwa mara mawasiliano ya simu bila kusimamiwa.
13. Mgonjwa atakuwa huru kushiriki katika shughuli za makundi yoyote ya kijamii, kidini, na vikundi vya jamii, isipokuwa wakati kufanya hivyo kutaingilia haki za wagonjwa wengine.
14. Mgonjwa atakuwa huru kuhifadhi na kutumia mavazi yake binafsi na vitu vingine kama hivyo nafasi ikiwepo, mradi kufanya hivyo hakutaingilia haki za wagonjwa wengine.
15. Mgonjwa atakuwa na haki ya faragha anapotembelewa na, kama amefunga ndoa, kushiriki chumba kimoja na mmewe au mkewe kama wote wawili wamelazwa katika hospitali sawa na wamekubaliana hivyo, isipokuwa wakati hairuhusiki kimatibabu na hayo kunakiliwa na daktari katika kumbukumbu. Mgonjwa ana haki ya kuishi na kupata huduma katika hospitali na ruhusa ya kuridhisha yakutimiza mahitaji na mapendeleo ya kibinafsi, ikiwa ni pamoja na kuchagua chumba na mshiriki chumba, isipokuwa wakati afya na usalama wake au wa wagonjwa wengine utakuwa hatarini.
16. Mgonjwa hatakatazwa huduma zinazofaa kwa vigezo vya kuangalia umri, jinsia, utambulisho wa jinsia, mwelekeo wa kingono, mbari, rangi, hali ya ndoa, hali ya familia, ulemavu, dini, asili ya kitaifa, chanzo cha mapato, chanzo cha malipo au taaluma.
17. Mgonjwa atakuwa na haki ya kutibiwa na daktari atakaye mchagua, mradi haya yatazingatia kanuni na sheria za hospitali kuhusiana na njia za uidhinishaji za hospitali yenyewe.
18. Mgonjwa atakuwa na haki ya kuwa na wazazi wake, kama yeye ni mtoto, au mwenziwe wa ndoa, au jamaa wa pili, au mwakilishi wa kibinafsi, kama ni mtu mzima, akimtembelea hospitalini, bila vizuizi, kama mgonjwa atachukuliwa kuwa na ugonjwa usioponyeka kulingana na daktari anayehusika kumhudumia.
19. Mgonjwa atakuwa na haki ya kupokea wawakilishi wa mashirika yaliyoidhinishwa kwa mujibu wa RSA 151:28.

20. Mgonjwa hastahili kunyimwa fursa ya kulazwa katika kituo ikizingatiwa kwamba *Medicaid* ndiyo chanzo kimsingi cha malipo yake ikiwa nafasi itapatikana.
21. Kulingana na vigezo na masharti ya bima ya wagonjwa, mgonjwa atakuwa na ufikio kwa mtoa huduma yeyote katika mtandao wa bima yake na rufaa kwa mtoa huduma au huduma iliyo ndani ya mtandao huo haitazuiliwa kwa mujibu wa RSA 420-J:8, XIV.
22. Mgonjwa hatakatazwa kulazwa, kutunzwa au kupata huduma kwa kuzingatia hali ya chanjo ya mgonjwa.
23. Usaidizi wa mgonjwa.
- (a) Mbali na haki zilizoainishwa katika aya ya 18, mgonjwa atakuwa na haki ya kuteua mwenzi, mwanafamilia au mlezi ambaye anaweza kutembelea kituo wakati mgonjwa anapokea huduma. Mgonjwa ambaye ni mtoto anaweza kutembelewa na mzazi, mlezi au mtu anayechukua nafasi ya mzazi kwenye kituo hicho wakati anahudumiwa.
- (b) Vighairi:
- (1) Bila ya kujali aya ndogo ya (a), kituo cha huduma ya afya kinaweza kuweka sera za matembezi zinazopunguza au kuzuia matembezi, wakati:
- (A) Kuwepo kwa wageni kunaweza kuzuiliwa kiafya au kimatibabu katika uamuzi bora wa kimatibabu wa wataalamu wa afya;
- (B) Kuwepo kwa wageni kunaweza kuingilia utunzaji au haki za mgonjwa yeyote;
- (C) Wageni wanajihusisha na tabia ya usumbufu, vitisho au vurugu kwa mfanyakazi yeyote, mgonjwa au mgeni mwingine; au
- (D) Wageni hawazingatii sera iliyoandikwa ya hospitali.
- (2) Kwa ombi, mgonjwa au mwakilishi wa mgonjwa, ikiwa mgonjwa hana uwezo, atapewa sababu ya kunyimwa au kubatilisha haki za kumtembelea chini ya aya hii.
- (c) Kituo cha huduma ya afya kinaweza kuhitaji wageni kuvaa vifaa vya kujikinga vinavyotolewa na kituo hicho au vinavyotolewa na mgeni na kuidhinishwa na kituo hicho. Kituo cha huduma ya afya kinaweza kuhitaji wageni kuzingatia itifaki na kanuni za maadili zinazofaa. Kituo cha huduma ya afya kinaweza kubatilisha haki za kutembelewa kwa kushindwa kutii aya hii ndogo.
- (d) Hakuna chochote katika aya hii kitakachotafsiriwa kuhitaji kituo cha huduma ya afya kumruhusu mgeni kuingia katika chumba cha upasuaji, chumba cha kujitenga, kituo cha kutengwa, mazingira ya afya ya kitabia au eneo jingine ambalo kwa kawaida limezuiliwa au kubaki wakati wa usimamizi wa huduma ya dharura. Hakuna chochote katika aya hii kitakachotafsiriwa kuhitaji kituo cha huduma ya afya kumruhusu mgeni kuingia zaidi ya vyumba, vitengo au wodi ambayo mgonjwa anapokea huduma au zaidi ya maeneo ya kawaida katika kituo cha huduma ya afya.
- (e) Haki zilizoainishwa katika aya hii hazitasitishwa, kusimamishwa au kuondolewa na kituo cha huduma ya afya, idara ya afya na huduma za binadamu au taasisi yoyote ya serikali, bila kujali tangazo la dharura lililotangazwa na gavana au bunge. Hakuna kituo cha huduma ya afya kilichoidhinishwa kwa mujibu wa RSA 151:2 kitakachohitaji mgonjwa aache haki zilizotajwa katika aya hii.
- (f) Kila kituo cha afya kilichopewa leseni kwa mujibu wa RSA 151:2 kitachapishwa kwenye tovuti yake:

- (1) Nyenzo za habari zinazoelezea haki zilizotajwa katika aya hii;
 - (2) Hati ya haki za wagonjwa ambazo zinatumiwa kwa kituo kwenye tovuti yake; na
 - (3) Sera ya kutembelea hospitali inayoeleza kwa kina haki na wajibu uliotajwa katika aya hii na mipaka iliyowekwa juu ya haki hizo na sera iliyoandikwa ya hospitali kwenye tovuti yake.
- (g) Isipokuwa kama inavyotakiwa na sheria au kanuni za shirikisho, idara au wakala mwingine wowote wa serikali hautachukua hatua yoyote inayotokana na aya hii dhidi ya kituo cha huduma ya afya kwa:
- (1) Kumpa mgeni fursa ya kufikia jengo au eneo linalodhibitiwa na kituo cha huduma ya afya;
 - (2) Kushindwa kulinda au kuhakikisha usalama au faraja ya mgeni anayepewa ufikiaji wa jengo au eneo linalodhibitiwa na kituo cha huduma ya afya;
 - (3) Vitendo au kutotenda kwa mgeni yeyote anayepewa ufikiaji wa jengo au eneo linalodhibitiwa na kituo cha huduma ya afya.

Wakati wowote ukiwa na maswali, mahitaji, au malalamishi kuhusu kiwango cha utunzaji au huduma iliyotolewa, twakuhimiza uweze kuyaleta kwa haraka kwa mwanachama yeyote wa Timu ya Utunzaji.

Wafanyikazi wetu wa Husiano za Wagonjwa wako tayari kujadiliana na kutazama kwa kina zaidi malalamishi au mahitaji yoyote uliyo nayo. Maswali yako yatashughulikiwa kwa njia ya kifaragha. Wanachama wa Husiano za Wagonjwa waweza kufikiwa kupitia kwa simu kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa, saa 2.00 asubuhi hadi saa 10.00 jioni (8am-4pm) katika nambari (603)230-1902, TTY: (603) 228-7135, au kwa barua kupitia anwani ptrelations@crhc.org au kwa maandishi, katika Concord Hospital Patient Relations, 250 Pleasant St., Concord, NH 03301.

Unaweza pia kuwasilisha matatizo kwa: **Jimbo la New Hampshire:** Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu ya New Hampshire, Shirika la Usimamizi wa Huduma za Afya Utawala Main Building, 129 Pleasant Street, Concord, NH 03301, [\(603\) 271-9039](tel:6032719039) au hfa-licensing@dhhs.nh.gov; **Uidhinishaji wa Hospitali:** DNV Healthcare USA Inc., Kwa: Healthcare Complaints (Malalamiko kuhusu Huduma ya Afya), 1400 Ravello Dkt Katy, TX 77449, tovuti: <https://www.dnvhealthcareportal.com/patient-complaint-report>, barua pepe: hospitalcomplaint@dnv.com, [1-866-496-9647](tel:1-866-496-9647), au faksi: [\(281\) 870-4818](tel:2818704818), **Kwa Wagonjwa wenye Medicare Pekee:** Acentra Health, BFCC-QIO Mpango, 5201 West Kennedy Blvd. Suite 900, Tampa, FL 33609, [1-888-319-8452](tel:1-888-319-8452), au TTY [1-855-843-4776](tel:1-855-843-4776).